**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI**

**SHULE YA SEKONDARI MWANZI**


**SHULE YA SEKONDARI MWANZI**

**S.L.P 37**

**MANYONI**

**12.06.2023**

**MKUU WA SHULE – 0783 84 29 00**

**MAKAMU MKUU WA SHULE – 0769 37 25 97**

**MATRON/PATRON – 0672 76 11 57/0752 05 34 54**


**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWANZI HALMASHAURI YA MANYONI, MKOA SINGIDA 2023.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya HGL.

Shule ya Sekondari MWANZI ipo umbali wa Kilometa 1.5 Mashariki mwa Halmashauri ya Mji wa Manyoni. Usafiri wa bodaboda/bajaji unapatikana katika

kituo cha mabasi Manyoni Nauli ni Shiling 2000 kwa pikipiki na Shilingi 3000 kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 03/07/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 04/07/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 20/07/2023

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 SARE ZA SHULE

a) Suruali mbili za Dark Blue zenye celebration mbili kila upande, **zisizobana** kwa wavulana.
b) Sketi mbili ndefu za Dark Blue zenye mshono wa V mbele, **zisizobana** kwa wasichana.
c) Shati nyeupe mbili za mikono mirefu.
d) Hijabu nyeupe za coton zisizo na urembo wowote (kwa wasichana wa Kiislamu)
e) Sweta za kijivu zenye shingo ya V (zitapatikana shuleni)
f) T-shirt za rangi ya njano zenye nembo ya shule. (zinapatikana shuleni)
g) Tai za special za blue zenye strips nyeupe (zitapatikana shuleni)
h) Viatu vya Kamba vyeusi vyenye visigino vifupi.
i) Soksi **nyeusi** kwa wavulana na **nyeupe** kwa wasichana.
j) Mkanda wa Ngozi mweusi kwa wavulana.
k)

**NGUO ZA KUSHINDIA**

a) Suruali mbili nyeusi zenye celebration mbili kila upande zisizobana.
b) Wasichana magauni mawili marefu ya **light blue** ya kitambaa cha coton mshono wa solo na mikono ya shati.
c) T-shirt mbili zenye nembo ya shule (zitapatikana shuleni).
d) Track-suit nyeusi zenye strips nyeupe kwa ajili ya michezo.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

a) Ream ya karatasi A4 moja (**DOUBLE A**) kwa kila muhula (zitapatikana duka la shule)
b) Vitabu vya masomo ya tahasusi ya (**HGL**) na Dictionary
c) Godoro la futi mbili na nusu
d) Mashuka mawili ya cotton ya **pink** kwa wasichana na **light blue** kwa wavulana.
e) Blanket moja
f) Chandarua
g) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
h) Ndoo ndogo mbili zenye mifuniko (zitapatikana duka la shule)
i) Dawa ya chooni lita 5 (zitapatikana duka la shule)

j) Wasichana waje na Reki (zitapatikana duka la shule), Panga, fagio la brashi laini (zitapatikana duka la shule), chelewa na mopper.
k) Wavulana waje na jembe lenye mpini (zitapatikana duka la shule), kwanja, fagio la brashi gumu, chelewa na mopper.
l) Sanduku la bati
m) Box file kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake shuleni (zitapatikana duka la shule)
n) Madaftari makubwa (counter books) 7 au Zaidi (zitapatikana duka la shule), mkebe, kalamu za wino, za risasi na rula.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Original Result slip ya kidato cha nne.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

***ELIMU NI MAISHA***

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MWANZI

__________________

BENAS DICKSON MAGAFU

**MKUU WA SHULE**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0783 84 29 00**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0769 37 25 97**
- **Mwandamizi Taaluma 0623 21 65 65**
- **Mwandamizi Malezi 0683 900 875**

# FOMU YA MAKUBALIANO NA UTAMBULISHO

**A. HABARI ZA MWANAFUNZI**

| PICHA YA MWANAFUNZI |
|---|

I. JINA LA MWANAFUNZI: ________________________________________

II. TAREHE YA KUZALIWA: ________________ WILAYA _________________

III. DINI _______________________ DHEHEBU ______________________

MAHALI ATAKAPOKUWA ANAKWENDA LIKIZO

I. JINA _____________________ UHUSIANO __________ MAHALI ______________

II. JINA _____________________ UHUSIANO __________ MAHALI ______________

**KUKUBALI NAFASI**

Mimi ____________________________ mimesoma maelekezo ya kujiunga na shule ya sekondari MWANZI. Nakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni Pamoja na kutii sheria za shule. nitakapokuwa shuleni, nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kusoma kwa bidi na kuchapa kazi za mikono kwa bidi ili kutimiza lengo la kupata elimu katika ujumla wake.

**Saini _________________ Tarehe ___________________**

**B. HABARI ZA MZAZI/MLEZI**

| PICHA YA MZAZI |
|---|

I. JINA KAMILI _____________________________________

II. AINISHA KAMA NI MZAZI AU MLEZI ____________________

III. UHUSIANO ULIOPO NA MWANAFUNZI (KAMA SIO MZAZI) _____________

IV. KAZI YAKE ________________

V.

VI. ANWANI YA KAZINI __________________

VII. NAMBARI YA SIMU ___________________

VIII. ANWANI YA NYUMBANI ___________________

IX. UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI
Nimehakikisha maelekezo na maagizo yameeleweka na mtoto wangu atafuata sheria na taratibu zote za shule ya sekondati Mwanzi.

**Jina _____________________ sahihi _________________ Tarehe _________________**

JINA LA AFISA MTENDAJI WA KATA/KITONGOJI/MTAA ________________________

SAINI _______________________

TAREHE _____________________

MUHURI WA OFISI _______________

**FOMU HII NA FOMU YA MEDICAL EXAMINATION ZIRUDISHWE SHULENI ZIKIWA ZIMEJAZWA KIKAMILIFU**

# MANYONI DISTRICT COUNCIL

MWANZI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 37
MANYONI
DATE: ……………………………..

To the medical officer at
…………………………………………
…………………………………………
…………………………………………..
Dear Sir/Madam

**REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine MR./Miss ……………………………………………………………………………….. as to his/her fitness as a full-time student of MWANZI SECONDARY SCHOOL, may I kindly ask you to fill in the particulars in the form hereunder.

Yours Sincerely

………………………

BENAS D. MAGAFU
HEADMASTER

**TO BE COMPLETED BY THE MEDICAL OFFICER**

1. Blood count (white Blood cells) …………………………………………………
2. Stool examination …………………………………………………
3. Urine examination …………………………………………………
4. Gestation (for girls only) …………………………………………………
5. Venereal disease …………………………………………………
6. TB test …………………………………………………
7. E.N.T Problems …………………………………………………
8. Defects of a) The left and right eye …………………………………………………
   b) The chest …………………………………………………
9. Any CHRONIC or FAMILY disease e.g., Epilepsy, Sickle cell etc ………………………………………………….

DECLARATION

I have examined MR/MISS ………………………………………………………………. and certify that he/she is physically fit/unfit to pursue his/her studies as stated above.

…………………………………………..
Signature of Medical officer
…………………………………………..
Name of Medical officer
Designation ………………………………………….. official stamp ………………………………………………….